

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule,
Wilaya ya Iringa,
S.L.P 984,
IRINGA.
31/05/2019.

TANGAZO LA KUTAFUTA WASAFIRISHAJI WA MADINI YA UJENZI KWA AJILI YA KAZI YA UJENZI WA OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE WA WILAYA YA IRINGA.

Kazi Na.UKW/IRV/V.2002/UJ/OUT/02

Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) Iringa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imepokea fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa ofisi ya Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya ya Iringa. Ujenzi huo utatekelezwa kwa kuwatumia mafundi kwa utaratibu wa "Force account". Hivyo, Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule wa Wilaya ya Iringa anawatangazia Vikundi na Wasafirishaji wote wenye sifa kwa ajili ya kuomba kufanya kazi tajwa hapo juu.

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Muombaji awe na Mitambo/Gari aina ya Tipper yenye ukubwa wa mita za ujazo kuanzia nne (4) na kuendelea (Cubic mitre), ambayo itatumika katika usafirishaji wa Mawe, Mchanga, Kokoto na Kifusi.
2. Muombaji atatakiwa kuwa na wapakiaji wa Mawe, Mchanga na Kokoto katika Gari aina ya Tipper yenye ukubwa wa mita za ujazo kuanzia nne (4) na kuendelea (Cubic mitre) na atatakiwa kupakia na kusafirisha hadi eneo la Mradi wa ujenzi wa ofisi ya Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) Iringa katika eneo la Mawelewele (karibu na msikiti wa ASAS), Kata ya Mwangata-Manispaa ya Iringa.

3. Muombaji atatakiwa kuomba malipo mara baada ya kukamilisha kazi aliyopangiwa ndani ya siku saba (7).
4. Muombaji anaruhusiwa kuomba kazi mojawapo ya usafirishaji kati ya Mawe au Mchanga au Kokoto au vyote kwa pamoja.
5. Muombaji atatakiwa kuonesha bei au gharama ya usafirishaji wa Mawe, Mchanga na Kokoto kutoka eneo analochukulia hadi eneo la Mradi kwa tripu moja.
6. Muombaji atakayekidhi vigezo atatakiwa kukaguliwa na Mtaalam akishirikiana na Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi walio eneo la mradi kabla ya kushusha Mawe, Mchanga na Kokoto, endapo hatakaguliwa kazi hiyo haitalipwa.
7. Halmashauri inaweza kufuta maombi ya kazi uliyoomba pale ambapo kutakuwa na sababu za msingi, mfano; bei kuwa juu kupita gharama halisi ya soko, maombi ya kazi uliyoomba kushindwa kukidhi vigezo, kujihusisha na aina yoyote ya udanganyifu au rushwa.
8. Msafirishaji awasilishe uthibitisho wa kutokuwa ametenda kosa la kijinai, kuwa na mgogoro na serikali
9. Msafirishaji atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na vitendea kazi muhimu vitakavyo mwezesha kukamilisha kazi husika (Mfano: -Gari la TANI 7 (4M³) na vinginevyo.
10. Fomu ya usafirishaji wa madini ya ujenzi inapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU), MAKAO MAKUU YA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 108, IRINGA) iliyopo katika Jengo la SIASA NI KILIMO, MTA A WA GANGILONGA, kuanzia tarehe 31/05/2019 hadi tarehe 06/06/2019, katika muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa.
11. Maombi ya kazi ya usafirishaji wa madini ya ujenzi yatawasilishwa kwa kujaza fomu ya usafirishaji wa madini na kuambatishwa pamoja na barua ya maombi.
12. Maombi ya kazi ya **USAFIRISHAJI WA MADINI YA UJENZI** yaandikwe kwa herufi kubwa yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au

Kikundi na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha, bahasha ifungwe vizuri. Juu ya bahasha landikwe Jina la kazi uliyoomba, Namba ya kazi husika na Anuani ya (KATIBU WA KAMATI YA MANUNUZI, UJENZI WA OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE WA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 984, IRINGA)

13. Maombi yote katika nakala **halisi moja (1)** na **nakala kivuli moja(1)** yaletwe kwenye Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU), MAKAO MAKUU YA WILAYA YA IRINGA, S.L.P 108, IRINGA) iliyopo katika Jengo la SIASA NI KILIMO, MTAA WA GANGILONGA. Muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.
14. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 06/06/2019, saa 4.00 asubuhi na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.
15. Maombi yote ya kazi za usafirishaji yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.
16. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuwezesha kujaza makabrasha itakuwa tarehe 01/06/2019 (Jumamosi). Waombaji wote wafike saa 3.00 kamili asubuhi katika jengo la SIASA NI KILIMO - Gangilonga ili kwenda kuona eneo ulipo mradi Mawelewele karibu na msikiti wa ASAS, kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.
17. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hii katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

.....
**MWENYEKITI WA KAMATI YA UJENZI
OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE
WILAYA YA IRINGA**